# HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. DR. ANGELINE MABULA (MB), WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWENYE MAHAFALI YA AROBAINI NA MOJA (41) YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO TAREHE 14/04/2023

Mhe. Fatuma Mwassa, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro;

Mhe. Prof. Ernest Kihanga, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo Cha Ardhi Morogoro;

Bw. Seushi Mburi, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Bw. Charles Sospeter Saguda, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro;

Wajumbe wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Wakuu na Watendaji wote wa Taasisi na Idara za Serikali mliopo hapa;

Wajumbe wa Menejimenti ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Ndugu Wanahabari kutoka Vyombo Mbalimbali Vya Habari;

Wageni Waalikwa Wote, Mabibi na Mabwana,

**Habari za Asubuhi!**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Awali ya yote, ninapenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kufika hapa kwa ajili ya mahafali ya arobaini na moja (41) ya vijana wetu. Aidha, kipekee ninakushukuru wewe Mwenyekiti na Bodi yako kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika mahafali haya. Hali kadhalika ninachukua fursa hii adhimu kuwashukuru viongozi na wageni wote kwa kuitikia wito wa kuja kuungana nasi katika shughuli hii muhimu.

**Ndugu Mwenyekiti**

Kipekee pia ninapenda kumpongeza Mkuu wa Chuo pamoja na Menejimenti ya Chuo, Walimu na Watumishi wote wa Chuo kwa ushirikiano na uwajibikaji wenu mzuri kwani ndio umewezesha kupatikana wahitimu hawa 330 waliopo mbele yetu tunaowatunuku vyeti leo. Ni Dhahiri kuwa, bila ya kuwepo uwajibikaji wenu wa pamoja katika kutekeleza majukumu ya Chuo leo tusingekuwa hapa kwenye mahafali haya. Ni kutokana na umoja wenu, mshikamano, na nia thabiti ya kutekeleza wajibu wenu ndiyo sababu leo tuko hapa tukiwa na furaha kubwa ya kusherehekea na wahitimu wetu wa mwaka 2021/2022.

**Ndugu Mwenyekiti**

Mwisho, pongezi zangu hazitakuwa zimekamilika kama sitawashukuru na kuwapongeza kwa dhati wahitimu wetu kwa kufuzu na kuhitimu vyema masomo yao. Ninafahamu kuwa, elimu mliyoipata hapa chuoni katika mihula yote ya Chuo mtaitumia ipasavyo katika kuleta mabadiliko chanya na hatimaye kuleta maendeleo endelevu katika sekta yetu ya ardhi.

**Ndugu mwenyekiti,**

Wizara ya Ardhi na Taifa kwa ujumla vinatambua mchango mkubwa unaotolewa na Chuo cha Ardhi Morogoro katika sekta ya ardhi hasa katika kuzalisha wataalamu wa fani za Upimaji Ardhi na Mipango Miji katika ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada. Juhudi zenu tunaziona na tunaziunga mkono.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kuanzishwa kwa Chuo hiki kulitokana na nia njema ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujitegemea katika uzalishaji raslimali watu wenye ujuzi na weledi wa kutekeleza majukumu yao ili kukidhi mahitaji ya soko la kazi, hasa katika Sekta ya Ardhi nchini. Sheria ya Bunge Na. 35 (Sura 122) ya mwaka 1974 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2009) imebainisha wazi majukumu ya Chuo, kwa kutaja baadhi ni kama yafuatayo:

a) Kuandaa miundombinu na mazingira ya kujifunzia na kufundishia misingi, kanuni na mbinu za utendaji katika fani za **upimaji ardhi**, **mipango miji na vijiji, usimamizi na uthamini wa ardhi, usanifu wa majengo** na fani nyingine ambazo Bodi itaona zinafaa; na
b) Kuendesha programu za mafunzo ya masomo yaliyotajwa hapo juu na masomo mengine ambayo Bodi itaona yanafaa;

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kama ilivyobainishwa katika hotuba yako na ya Mkuu wa Chuo, katika miaka 46 tangu kuanzishwa kwake, Chuo hiki kimejipanua, lakini kwa kasi ndogo. Hili limetokana na kutokutimiza kikamilifu wajibu wenu wa kisheria ambapo katika kipindi cha miaka 40 mlifundisha fani ya aina moja tu. Hata hivyo, nimefarijika kuona kwamba maandalizi ya Mpango Kabambe yamekamilika. Mpango huu unabeba maono ya taasisi kwa miaka 20 ijayo (yaani 2023 – 2043).

**Ndugu Mwenyekiti,**

Nitumie nafasi hii kuwaahidi kwamba Wizara yangu itakuwa nanyi bega kwa bega katika utekelezaji wa Mpango Kabambe mliouandaa. Mpango huu unaenda sambamba na maelekezo ya Chama cha Mapinduzi kupitia Ilani yake katika Uchaguzi wa mwaka 2020, iliyolenga kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote kwa kuzingatia falsafa ya kujitegemea yenye kuendana na mazingira ya nchi yetu, hususan elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Mnafahamu juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan za kujenga madarasa 15,000 kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 jinsi zilivyochagiza ongezeko la udhili katika shule za sekondari. Hivyo basi, Mpango Kabambe ukitekelezwa utawezesha kuongeza nafasi za wahitimu wa kidato cha nne na sita kujiendeleza katika ngazi za Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada.

**Ndugu Mwenyekiti**

Majukumu ya Wizara ya Ardhi ni kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kisheria. Majukumu haya yanatekelezwa kwa kutumia raslimali watu yenye ujuzi na weledi wa hali ya juu iliyoandaliwa vizuri katika vyuo vyetu vya hapa nchini kama kilivyo Chuo cha Ardhi Morogoro. Katika Sekta ya Ardhi bado kuna changamoto kubwa ya uwepo wa rasilimali watu iliyo bora na wenye weledi wa hali ya juu. Hivyo, ni imani yangu kuwa, wahitimu wetu wa mwaka huu hamtatuangusha katika utekelezaji wa majukumu yenu.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Wizara ya Ardhi itaendelea kubuni, kusimamia na kupanga matumizi bora ya ardhi kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo kwa nia ya kuboresha maisha ya Watanzania na kupunguza migogoro ya ardhi na hatimaye kuitokomeza kabisa. Tutaendelea kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria za ardhi, upangaji, upimaji, na utatuzi wa migogoro pamoja na kanuni, na taratibu na miongozo mbalimbali.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Zipo faida nyingi za kupanga, kupima na kumiliki ardhi kisheria. Naomba kutaja kwa ufupi faida hizo:-

i. Ardhi iliyopangwa, kupimwa na kumilikiwa kisheria inajulikana ukubwa wake halisi, mahali ilipo na ni salama kwani haina migogoro ya mipaka, matumizi yake na hata umiliki wake.
ii. Ardhi iliyopangwa, kupimwa na kumilikiwa kisheria ni mtaji na dhamana katika vyombo vya fedha na sheria nchini.
iii. Ardhi iliyopangwa, kupimwa na kumilikiwa kisheria ni rahisi kwa serikali, mashirika na taasisi kuweka miundo mbinu ya kisekta kama maji, umeme na barabara;
iv. Ardhi iliyopangwa, kupimwa na kumilikiwa kisheria ni kitovu cha uwekezaji wa ndani na nje.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Sambamba na faida nilizotaja hapo juu ninatambua pia kuwa zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi linahitaji fedha nyingi. Hivyo ninachukua fursa hii kuwahamasisha wananchi kuchangia gharama za upangaji, upimaji ardhi na uandaaji wa hati miliki. Ninatoa wito pia kwa Wizara na wadau wote muhimu kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuandaa mipango ya jumla na ya kina ya uendelezaji miji, upimaji wa maeneo ya kutosha kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Inaeleweka kwa wananchi wengi sasa kuwa, ardhi iliyopangwa, kupimwa, kumilikishwa kisheria ambayo ni dhahiri huwekewa miundombinu na huduma stahiki kwa maendeleo yao; ni chachu ya wananchi hao kuhamasika kulipa kodi yao ya pango la ardhi. Kodi hizi  zimeainishwa kisheria, hivyo naomba wamiliki wote wa ardhi kote nchini kulipa kodi za ardhi kwa wakati muafaka.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Inafahamika pia kuwa, kodi za ardhi ni chachu ya maendeleo ya Taifa na upatikanaji wa uhakika wa huduma za kijamii. Serikali itaendelea kutoa msukumo kwa wamiliki wote kulipa kodi ya majengo pamoja na ya pango la ardhi. Ujumbe wangu kwa wananchi ni "Lipa kodi ya ardhi uwe na uhakika wa dhamana, mtaji na mikopo kwani ardhi isiyolipiwa kodi haikopesheki".

**Ndugu Mwenyekiti,**

Changamoto zilizoainishwa katika hotuba ya Mwenyekiti wa Bodi, hotuba ya Mkuu wa Chuo pamoja na Risala ya Wanafunzi ni za msingi. Nasema, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya Chuo cha Ardhi Morogoro hatua kwa hatua kadri bajeti itakavyoruhusu.

## HITIMISHO

**Ndugu Mwenyekiti,**

Mwisho, ninachukua nafasi hii tena kuwashukuru sana uongozi wa Chuo kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika mahafali haya ya arobaini. Aidha, ninaendelea kuwashukuru pia wazazi kwa kugharamia ada za mafunzo ya watoto wao hadi leo wameiva sasa kulitumikia Taifa lao kupitia ujuzi walioupata hapa. Niwashukuru pia wafanyakazi na wanajumuiya wote wa Chuo cha Ardhi Morogoro kwa kuendelea kuchapa kazi kwa bidii.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Niwashukuru wahitimu nitakaowatunuku vyeti sasa na kuwaasa kuwa, muoneshe weledi katika kutumia utaalamu mlioupata hapa kwa manufaa mapana na ustawi wa sekta yetu ya ardhi. Aidha, epukaneni na utashi binafsi kwa kuzifuata ipasavyo sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa katika kutekeleza majukumu yenu. Epukeni rushwa, ufisadi na mjikinge na ugonjwa hatari wa ukimwi kwani bado nguvu kazi zenu tunazihitaji sana.

**Ndugu Wahitimu,**

Endeleeni sana kutafuta elimu kwani elimu haina mwisho. Kimsingi mnaposherehekea leo mahafali yenu haya, huu ni mwanzo tu katika taaluma. Hivyo, ninawaasa mtumie fursa ya sifa mlizozipata chuoni hapa kujiendeleza zaidi kielimu, kwa kujiunga na vyuo vinavyotoa elimu ngazi ya shahada katika fani zenu.

Mwisho kabisa, kwa wanafunzi mnaobaki naomba muongeze bidii ya masomo, dumisheni nidhamu, amani, utulivu na ushirikiano na wakufunzi wenu, kwani huo ndiyo msingi wa mafanikio yenu kitaaluma.

**Nawatakieni nyote sherehe njema na baraka tele katika kuendeleza Chuo chetu na Taifa letu kwa ujumla.**

**Asanteni kwa kunisikiliza.**

**Na sasa niko tayari kuwatunuku vyeti wahitimu wa leo.**